

## 16A-Idghaam Al-Mutamaathilayni (Zinazofanana)

### 1. إِذْغَامُ الْمُتَمَاثِلِينَ Idghaam Al-Mutamaathilayni (Zinazofanana)

At-tamaathul katika Tajwiyd maana yake ni: kuweko herufi mbili za jinsi moja zenyen makhraj moja na swiffah moja.

(Idghaam Al-Mutaamathilayni) ni kukutana herufi mbili zinazofanana na zinazotoka katika makhraj moja na zina swiffah moja. Herufi mbili hizo zinapokutana, kwa sharti kuwa herufi ya kwanza kuwa saakin na ya pili huwa na *i'raab*; hapo huwajibika idghaam kwa kuingizwa herufi ya kwanza kwenye herufi ya pili na kupelekea kupatikana shaddah na ni sawa zikiwa herufi mbili hizi ziko kwenye neno moja au maneno mawili

Suwrah/ Ayah	Matamshi	Mifano	Herufi
Al-Baqarah (2: 60)	<b>idhwri<b>b-b</b>i'aswaakal-hajar<sup>1</sup></b>	أَضْرِبْ بِعَصَالَكَ الْحَجَرَ	ب
An-Naml (27: 28)	<b>idh-hab<b>b</b>ikitaabiy</b>	أَذْهَبْ بِكَتَبِي	
al-Baqarah (2: 16)	<b>famaa rabihat-<b>t-t</b>ijaaratuhum</b>	فَمَا رَبَحَتْ تَجْرِيَتْهُمْ	ت
An-Naml (27: 43)	<b>maa kaana<b>t-t</b>a'budu min duwni-Allaah</b>	مَا كَانَتْ تَعْبُدُ مِنْ دُونِ اللَّهِ	
Al-Maaidah (5: 61)	<b>wa qaddakhaluw bil-kufr</b>	وَقَدْ دَخَلُوا بِالْكُفْرِ	د
Al-Israa (17: 33)	<b>falaa yusrif-<b>f</b>filqatl</b>	فَلَا يُسْرِفْ فِي الْقَتْلِ	ف
An-Nisaa (4: 78)	<b>yudrik-<b>k</b>kumul-mawtu</b>	يُدْرِكُمُ الْمَوْتُ	ك

<sup>1</sup>Al-Baqarah (2: 60)

Al-Furqaan (25: 10)	<b>wa yaj' al-llaka</b> Quswuwraa	<b>وَسَجَّلَ لَكَ قُصُورًا</b>	ل
Al-Baqarah (2: 33)	<b>alam aqul-lakum</b>	<b>أَلَمْ أَقُلْ لَكُمْ</b>	
al-Baqarah (2: 191)	<b>wa akhrijuwhum-mmin</b> haythu	<b>وَأَخْرِجُوهُمْ مِنْ حَيْثُ</b>	ه
Al-Ma'aarij (70: 27)	<b>walladhiyna hum-mmin</b> 'adhaabi rabbihim- <b>mmushfiqawn</b>	<b>وَالَّذِينَ هُمْ مِنْ عَذَابٍ</b> <b>رَبِّهِمْ مُشْفِقُونَ</b>	
AL-Insaan (76: 2)	<b>Innaa Khalaqanal-</b> insaana min- <b>nnutwafatin</b>	<b>إِنَّا خَلَقْنَا إِلَّا نَسَنَ مِنْ نُطْفَةٍ</b>	ن
Yuwsuf (12: 30)	<b>Turaawidu fataaha 'an-</b> <b>nnafsihi</b>	<b>تُرَاوِدُ فَتَاهَا عَنْ نَفْسِهِ</b>	
An-Nuwr (24: 33)	<b>wa man yukrih-hhunna</b>	<b>وَمَنْ يُكْرِهُنَّ</b>	ه

- i. Idghaam haiwajibiki inapokuwa herufi ya kwanza ni ya madd; ي و. Kwa maana ي Yenye madd haingizwi katika ي isiyo ya madd. Vile vile, haingizwi و yenye madd katika و isiyo ya madd kwa sababu hazitoki katika makhraj moja. Bali huingizwa ي isiyo ya madd katika iliyosare nayo, na pia و isiyo ya madd huingizwa katika iliyosare nayo kwa kuwa zote zinatoka makhraj moja.

Mfano wa kukosekana kuungana kwa makhraj	Mfano wa kuungana kwa makhraj	Herufi
ءَامَّتُوا وَعَمِلُوا	فَقَدِ آهَتَدَوا وَإِنْ تَوَلُّوا	و
الَّذِي يُوَسِّعُ		ي

ii. Inajuzu kuwa idghaam na idhwhaar katika hali ya kuunganisha<sup>2</sup> kauli ifuatayo kwa namna mbili:

**مَا أَغْنَى عَنِي مَالِيَةٌ هَلَكَ عَنِي سُلْطَانِيَّةٌ**<sup>3</sup>

- Idghaam: Kuingiza herufi ya هـ katika neno la kwenye katika neno la هـ na wakati huo itasomeka مـالـيـهـ هـ (maaliyahhalaka) .
- Idhwhaar: Kuidhihirisha herufi ya هـ katika neno la هـ na kuitenganisha na kinachofuatia kwa kupumzika kidogo na hii ndio ارجـحـ arjah (rai yenyne nguvu kabisa)

---

<sup>2</sup>Rejea mlango wa 'As-Sakt'

<sup>3</sup>Al-Haaqqah (69: 28-29)